

»Vidokezo vya ufugaji wa kuku wa siku moja«

Katika mchakato wa ufugaji wa kuku kwa ajili ya biashara, viwango vya juu vya vifo hupatikana katika hatua za awali. Hata hivyo, vifo vinaweza punguzwa kwa kutumia mbinu bora zinazohitajika katika.

Vifaranga huletwa kwenye banda wakati mahitaji yote kama vile masunduku ya karatasi, vyombo vya kunyweshea maji, chanzo cha joto, vyombo vya kulishia chakula nakadhalika yamewekwa kikamilifu ili kuzalisha kuku wingi, na wenye ubora wa juu.

Mahitaji ya kushughulikia vifaranga

Banda la kushughulikia vifaranga linapaswa kuwa na sura ya mviringo, bila pembe kali. Katika hili, tumia katoni za makaratasi kwenye banda kwa muda wa siku 7 za kwanza, na kisha weka maranda ya mbao.

Vile vile, lisha ndege kwa vitamini pamoja na dawa za kuua viini kwa siku 3 za kwanza ili kuponya kitovu, na kudhibiti mfadhaiko. Hakikisha kuna vyombo vya kunyweshea maji vya kutosha katika uwiano wa chombo 1 kwa ndege 50 na vyombo vya kulishia vifaranga katika uwiano wa chombo 1 kwa vifaranga 25.

Katika siku 3 za kwanza, wape vifaranga maji yaliyochanganywa na chakula cha vifaranga. Ongeza mafuta ya taa kwenye maji ili kudhibiti matatizo ya mmeng' enyo wa chakula. Baada ya siku 3, wape vitamini kwa siku 7 kisha uwachanje dhidi ya ugonjwa wa kideri.

Watolee mwanga wa kutosha usio mkali sana ili kudhibiti vifaranga kujikula. Taa lazima ziwapo saa 24 kwa wiki 3 za kwanza. Toa joto la kutosha linalohitajika katika bandala vifaranga. Chunguza vifaranga ili kudhibiti halijoto ipasavyo, na hakikisha unadumisha chanzo cha joto.

Hakikisha kuna nafasi ya kutosha kwa vifaranga.